# JARIDA LA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

Toleo la Mtandaoni: 12 | 15 Agosti, 2022 - TABORA | www.michezo.go.tz

## MABINGWA UMISSETA 2022 WATWAA MEDALI



Wizara_SanaaTz

# MABINGWA UMISSETA 2022 WATWAA MEDALI

15 Agosti, 2022




# Ubunifu na Usafi Kivutio UMISSETA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Michezo imeendelea kufanyika katika hatua ya Makundi kwa Wavulana na Wasichana. Michezo mbalimbali ikiwemo Mpira wa Wavu, mpira wa kikapu, Netiboli, na mpira wa mikono.

Ubunifu, nidhamu na usafi ni sehemu ya mashindano Katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) yanayoendelea Mkoani Tabora ambapo washiriki ambao ni wanafunzi wa shule za Sekondari hushiriki zoezi hilo kila asubuhi.

Mkoa wa Tabora ni mojawapo ya kivutio cha Ubunifu kwa bweni la wanafunzi wa kike kutoka mkoa huo kuchora Ranani ya Afrika Mashariki kwa kutumia kokoto Agosti 16, 2022.

Wanafunzi hao pia wametengeneza Bendera za nchi wanachama wa Jumuiya hiyo, na kubuni ukumbi unaotumika kuendesha Mikutano ya Jumuiya hiyo.

Mkoa mwingine uliofanya vizuri ni Mkoa wa Mwanza, baada ya Wanafunzi hao kubuni hospitali pamoja na wodi ya kulaza wagonjwa, huku pia wakionesha mandhari na malighafi zinazopatikana katika mkoa huo.

Kwa upande wa Mkoa wa Arusha ulionesha ubunifu mzuri, ambapo Wanafunzi wamebuni sehemu za vivutio vya maporomoko ya maji pamoja na Msikiti unaotumiwana Waislam katika Ibada.

Mikoa mingine iliyoshiriki zoezi hilo ni Dodoma, Manyara na Morogoro.










WARD


IRINGA CARGO



# Tabora na Kigoma Bingwa Kuruka Chini UMISSETA 2022

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Mkoa wa Kigoma umefanikiwa kubeba Medali katika mchezo wa kuruka chini upande wa Wasichana, huku Mkoa wa Kigoma umebeba Medali kama hiyo upande wa Wavulana, katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) mkoani Tabora.

Tabora imebeba Medali hiyo kupitia mwanafunzi Mwalu Madirisha aliyeruka umbali wa mita 4 kwa Sentimita 96, huku Mpaji Gibson wa Kigoma akiruka umbali wa mita 6 kwa Sentimita 34.

Mshindi wa pili upande wa Wavulana ni Elia Clement kutoka Arusha aliyeruka mita 6 kwa sentimita 17, huku msindi wa tatu ni Andrea Luhaga kutoa Mkoa wa Tabora aliyeruka mita 5 kwa sentimita 68.

Katika upande wa Wasichana, Mkoa wa Pwani umeibuka nafasi ya pili kupitia Elizabeth Keryaro aliyeruka mita 4 kwa sentimita 77, ambapo nafasi ya tatu imekwenda Tanga kupitia Hadija Ramadhani aliyeruka mita 4 kwa sentimita 73.

Mikoa mbalimbali iliyoshiriki mchezo huo ni pamoja na Singida, Simiyu, Dar es Salaam , Katavi, Shinyanga, Geita, Arusha na Dodoma.




# Bongo Flavour Yashika Kasi Sanaa za Maonesho UMISSETA

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Mashindano ya Muziki wa kizazi kipya maarufu kama Bongo Flavour, yamezidi kushika kasi kwa wanafunzi wa shule za sekondari kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kushindana katika fani ya sanaa.

Muziki wa Kizazi kipya umejumuishwa kwenye mashindano ya michezo kwa shule za sekondari nchini (UMISSETA 2022), ambayo mwaka huu yanafanyika kitaifa Mkoani Tabora, kwa lengo la kuwapa vijana nafasi ya kuonyesha vipaji vyao katika uimbaji.

Mashindano ya Bongo Flavour yalianza Agosti 14, 2022 kwa mikoa ya kundi A ambayo ni Arusha, Kagera, Dar es salaam, Simiyu, Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Kigoma pamoja na Tanga kuanza kushindana.
Agosti 15, 2022 ilihusisha mikoa inayounda kundi B ambayo ni Morogoro, Iringa, Lindi, Ruvuma, Shinyanga, Mbeya, Njombe na Kusini Unguja na ile ya kundi C lenye wawakilishi kutoka Pwani, Mtwara, Mwanza, Tabora, Rukwa, Katavi, Songwe na Geita.

Mikoa iliyoingia fainali ni Dar es salaam, Kagera na Dodoma kutoka kundi A, Mbeya, Manyara, Shinyanga kundi B huku Rukwa, Tabora na Mtwara zikiwakilisha kundi C.

Kufuatia mashindano hayo ya muziki wa kizazi kipya, kuonekana kuungwa mkono na wadau mbalimbali wanaojitokeza kufuatilia, wito umetolewa watendaji wanaohusika na masuala ya utamaduni kuhakikisha kwamba vipaji vinavyoonekana kwenye UMISSETA vinaendelezwa.

Bi. Janeth Elias ni Afisa Utamaduni Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, ameishauri Mikoa husika kupitia maafisa Utamaduni wa mikoa na Halmashauri kuwafuatilia wanafunzi hao, na kuwatafutia shughuli mbalimbali zinazohusu matamasha katika shughuli za kiserikali.

"Mikoa inapata ugeni na viongozi wa kiserikali kwenye maeneo yao, vijana wa shule watumike kuwapokea kupitia shughuli zao za sanaa lakini pia kuwepo mashindano ndani ya Halmashauri na mikoa ili kuendelea kutunza vipaji vya watoto hawa"

"Hii itasaidi kuendeleza watoto wenye vipaji, na kuibua vingine vipya ndani ya Mikoa na Halmashauri kwa sababu watoto wataendelea kuona mwenzao akionekana wakati wa shughuli mbalimbali zinazohusisha viongozi akiwepo wa kitaifa kama Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu nk." Amefafanua Bi. Janeth.

**Riadha katika mbio za Relay kwenye Mashindano ya Michezo kwa Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) kitaifa mkoani Tabora wamepokea Medali zao Agosti 15, 2022 katika Uwanja wa Sekondari ya Wavulana Tabora.**






UMITASHUMTA
& UMISSETA
2022


32



045
55

**Michezo imeendelea kufanyika katika hatua ya Makundi kwa Wavulana na Wasichana. Michezo mbalimbali ikiwemo Mpira wa Wavu, mpira wa kikapu, Netiboli, na mpira wa mikono.**








# UMITASHUMTA | UMISSETA
## 2022

# #SensaBika

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

www.michezo.go.tz